# TAARIFA - KUMRADHI

Written by Administrator
Tuesday, 06 November 2012 13:58 - Last Updated Tuesday, 06 November 2012 14:21

VIEWED {hits}250{/hits} TIMES



Uongozi wa klabu ya Yanga unaomba radhi kwa taarifa zilizotolewa jana juu ya uteuzi wa meneja Shaban Katwila, Afisa Mawasiliano Baraka Kizuguto, habari ambazo zilitolewa na Kaimu Katibu Mkuu Lawrence Mwalusako.

Akiongea na waandishi wa habari makao makuu ya klabu makutano ya mitaa ya Twiga/Jangwani, Mwalusako amesema anaomba radhi kwa hali iliyojitokeza, kwani ameharakisha kutangaza uteuzi huo ambao bado ulikuwa haujadhibitishwa.

Unajua mtu anapoteuliwa kushika nafasi ya kazi, inapaswa kumpa taarifa mhusika kisha baada ya hapo mnakaa mwajiri na mwajiriwa kukubaliana mazingira ya utendeaji kazi na taratibu zingine, kitu hichi kilikuwa bado hakijafanyika hivyo vitakapo kua tayari tutawajulisha tena alisema 'mwalusako'

Kikao cha kamati ya utendaji kilikaa mwishoni mwa wiki na kupendekeza Katwila na Kizuguto kushika nafasi hizo, lakini taraibu za ufanyaji kazi wao zilikuwa bado hazijajdiliwa, hivyo hayo ndo makosa yaliyofanyika kuwatangaza rasmi ikiwa bado makubaliano hayafikiwa.